**TANGAZO LA SERIKALI NA…….LA TAREHE……………..**

**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)**

**SURA 287**

**SHERIA NDOGO**

***Zimetengenezwa Chini ya Kifungu cha 153(1)***

**SHERIA NDOGO ZA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA ZA MWAKA 2025**

| | | |
|---|---|---|
| Jina na Mwanzo wa Kutumika | 1. | Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka 2025 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. |
| Matumizi | 2. | Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. |
| Tafsiri | 3. | Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo:-<br><br>***"Afisa Mwidhiniwa"*** maana yake ni Mganga Mkuu wa Wilaya, Afisa Afya, Daktari wa Binadamu, Daktari wa Mifugo, Afisa Mifugo na Uvuvi, Afisa Afya Msaidizi, Afisa Mazingira, Afisa Mtendaji wa kata, Afisa Mtendaji wa Kijiji, Mkuu wa Soko, Mkaguzi wa Wilaya pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>***"Afya"*** maana yake ni hali ya kuwa mzima kimwili, kiakili na kijamii na si tu kutokuwepo kwa magonjwa au udhaifu.<br><br>***"Chakula"*** maana yake ni kitu chochote kinacholiwa na kunywewa na binadamu isipokuwa madawa, hii ni pamoja na:-<br>(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;<br>(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula; na<br>(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula (binzari n.k).<br><br>***"Choo cha kuvuta"*** maana yake ni choo ambacho kimejengwa na kuunganishwa na maji na kuwa na tanki ya kusukuma maji kwa ajili ya kuondoa uchafu hadi mahali palipoandaliwa.<br><br>***"Choo bora"*** maana yake ni choo chochote cha maji au cha shimo chenye kuta imara, iliyoezekwa, mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na chenye mfuniko kwenye |

RASIMU

tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, na shimo lililojengwa, lenye vipimo vya futi 4 x 3 na kimo cha futi 12 na zaidi.

***"Choo cha umma"*** maana yake ni choo kilichojengwa na Halmashauri au wakala wake kwa matumizi ya umma.

***"Eneo la wazi*** "maana yake ni eneo lililo chini ya Halmashauri ambalo limekatazwa kufanyia shughuli ambayo haihusiani na matumizi yaliyokusudiwa.

***"Halmashauri"*** maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

***"Hati ya usafi"*** maana yake ni hati itakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa inayothibitisha kukaguliwa kwa maeneo yote yaliyotajwa katika Sheria Ndogo hizi kulingana na Kanuni za Afya.

***"Jengo la biashara"*** maana yake ni jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kufanya biashara iliyokusudiwa.

***"Kaya"*** maana yake ni familia ya watu akiwemo baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo, au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba**.**

***"Kero au chukizo"*** maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, kimeota, kimekutwa au ni kichafu kiasi cha kusababisha:-

a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu.
b) harufu mbaya na kuudhi.
c) kuzaliana kwa wadudu na wanyama hatari kama vile nzi, mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari.
d) magonjwa kwa binadamu, kuhifadhi mbu, nzi, panya na viumbe hai wenye madhara.

*"**Kituo cha taka**"* maana yake ni eneo maalum lililotengwa kwa madhumuni ya kuweka taka ngumu kabla ya kusafirisha hadi kwenye dampo maalum lilitengwa kwa ajili ya kutupa taka hizo.

RASIMU

***"Maji taka"*** kama ilivyo katika Sheria ya Mazingira 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka kwenye makazi, taasisi, majengo ya biashara na viwandani.

*"**Mazao au mimea marefu**"* maana yake ni mazao au mimea inayozidi sentimita 15 kwenda juu kama vile Mtama, Mihogo, Mahindi, Mbaazi, Uwele na mengine yote yale yanayofanana na hayo.

***"Mkazi"*** maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri.

***"Mmiliki"*** maana yake ni mtu yeyote ambaye ana miliki ardhi, sehemu za starehe, nyumba za kulala wageni, nyumba za kuuzia vyakula, kumbi za starehe, mpangaji, wakala wa mpangishaji wa nyumba au jengo na makazi yoyote katika mtaa, endapo mazingira husika ni mtaa au barabara za mtaa.

***"Mkurugenzi"*** maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

***"Mzalishaji wa taka ngumu"*** maana yake ni mtu yeyote, kaya, taasisi, biashara, kiwanda ambaye katika kutekeleza shughuli zake huzalisha taka.

***"Pavement"*** maana yake ni sakafu imara ya mawe au matofali ya saruji au udongo yaliyochomwa na kujengewa kutoka katika nyumba hadi katika mfereji au barabara, kwa waendao kwa miguu au watazamaji wa vitu madukani.

***"Pipa la taka"*** maana yake ni chombo chochote chenye mfuniko kinachoweza kuhifadhi taka ngumu zinazozalishwa majumbani, sehemu za biashara, maofisini ili zisisambae na kuchafua mazingira na chenye ukubwa wa kuanzia urefu wa futi 3 na kuendelea na upana wa futi moja na nusu.

***"Taka"*** kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni kitu chochote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yoyote inayosababisha

RASIMU

uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

***"Taka Ngumu"*** kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani, katika majengo ya biashara, viwandani, gereji na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastiki au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps).

***"Taka za Majumbani"*** maana yake itajumuisha mabaki ya chakula, maganda ya matunda, majivu, kinyesi cha mifugo, taka za bustani, marapurapu ya nguo, karatasi za aina mbalimbali na vitu vingine ambavyo baada ya kuvitumia hutupwa.

***"Taka za Viwandani"*** kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, maana yake ni uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 sehemu ya IX.

***"Uchafu Hatari"*** kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni kitu chochote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira.

***"Uchunguzi wa Afya"*** maana yake ni hali ya mtu kupima afya yake kwa kuchukuliwa vipimo vya ndani na nje ya mwili ili kubaini kuwepo kwa vijidudu vya magonjwa vinavyoweza kuleta maambukizi.

***"Ufugaji wa ndani"*** maana yake ni ufugaji wa mifugo ndani ya eneo lililoruhusiwa tu.

***"Vyakula vya kupikwa au kukaangwa"*** maana yake inajumuisha maandazi, vitumbua, bagia chapati, mikate, samaki, chipsi, mihogo, viazi, ndizi, kuku na vinginevyo vinavyofanana na hivyo.

***"Wakala"*** maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira | 4. | (1) Ni wajibu wa kila mkazi au mfanyabiashara anayemiliki eneo la nyumba au biashara kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake kwa kuhakikisha kwamba:<br>a) majani yanayozunguka nyumba yake yanakatwa au kupaliliwa katika eneo lote hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake au eneo lake kwa wasio tazama barabarani.<br>b) takataka zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri.<br>c) takataka zinazokusanywa kwenye shimo lake na kuchomwa moto. |
| Kushiriki shughuli za usafi wa mazingira | 5. | 1) Halmashauri imetenga kila siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi na ama siku nyingine yoyote ambayo itamriwa na kutangazwa na Halmashauri kuwa ni siku ya wananchi wote kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri.<br>2) Ni wajibu wa kila mwananchi kuhakikisha kwamba anashiriki ipasavyo katika shughuli za usafi wa mazingira katika siku maalum zilizopangwa na Halmashauri na mwananchi atakayekaidi au atakayekataa kushiriki katika shughuli za kufanya usafi atakuwa ametenda kosa.<br>3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 5 cha Sheria Ndogo hizi ni wajibu wa kila mtu kuhakikisha maeneo yake binafsi ya makazi au biashara yanakuwa safi muda wote.<br>4) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au kiwanja au eneo lolote ambalo halijaendelezwa, kufanya usafi katika eneo hilo mara kwa mara ili kuondoa mazalia ya wadudu wasambazao magonjwa kwa binadamu, ikiwa ni pamoja na wanyama waharibifu na hatarishi kwa afya za binadamu. |
| Mimea mirefu | 6. | 1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kupanda au kuotesha mazao au mimea mirefu katika maeneo ya vijiji pamoja na maeneo mengine yaliyozuiliwa na Halmashauri. |
| Usafi wa mifereji | 7. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mifereji ya kupitisha maji inayozunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| | | na kuhakikisha mifereji hiyo inakuwa misafi na imara wakati wote.<br><br>2) Ni marufuku kuchomea takataka kwenye mifereji ya maji. |
| Kujenga pavement | 8 | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba kuweka sehemu ya waenda kwa miguu "*pavement*" mbele ya nyumba au biashara yake kwa kadri atakavyoelekezwa na Halmashauri.<br><br>2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka biashara ya aina yoyote aidha kwa kuuza au kwa maonyesho katika mfereji au katika pavement bila kwanza kupata kibali cha Halmashauri. |
| Uwekaji taa za nje majengo ya nyumba | 9. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki/mpangaji au mfanyabiashara wa nyumba za biashara kuweka taa enye/zenye mwanga wa kutosha nje ya nyumba au jengo la biashara analolitumia kwa shughuli yoyote na atatakiwa kuiwasha taa hiyo/hizo wakati wa usiku. |
| Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia ya wadudu. | 10. | 1) Ni wajibu wa mmiliki wa nyumba/mpangaji kuhakikisha kuwa hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu. |
| Upulizaji dawa za kuuwa wadudu/wanyama waharibifu | 11. | 1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha biashara ya upuliziaji dawa "*Fumigation*" au biashara ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika nyumba yoyote au mahali popote bila kuwa na mtaalam mwenye leseni hai kutoka Halmashauri na atasimamiwa na Afisa Afya wakati wa upulizaji. |
| Matengenezo na maegesho ya magari, pikipiki na mitambo | 12. | 1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.<br><br>2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuegesha magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi, barabarani na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njia hiyo.<br><br>3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo. |
| Usalama wa maji ya | 13. | 1) Ni wajibu wa kila mkazi kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa |

RASMI

| | | |
|---|---|---|
| kunywa. | | kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani cha maji. |
| Utengenezaji na uuzaji vyakula | 14. | 1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutengeneza, kuchoma, kupima, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote mtaani, uchochoroni, magengeni au kwenye nyumba yoyote au majengo ya taasisi ikiwemo Shule, zahanati vituo vya afya au jengo lolote la biashara hadi awe ametimiza masharti na kanuni za afya na amepata kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.<br><br>2) Ni wajibu wa kila mtu anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa kuhakikisha kwamba vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekwa kioo au lilitengenezwa kwa vioo ili kuzuia nzi, vumbi na wadudu waletao madhara ya afya kwa binadamu.<br><br>3) Ni marufuku kuuza vyakula au bidhaa zilizozuiliwa au zilizoisha muda wa matumizi.<br><br>4) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuuza vyakula vilivyopikwa na visivyopikwa vikiwa vimewekwa chini, vyakula vyote vitatakiwa kuwekwa juu ya meza ama vyombo maalum ambavyo ni visafi na ni wajibu wa muuzaji yeyote kuhakikisha kwamba eneo hilo la kuuzia vyakula ni safi wakati wote. |
| Uwezo wa afisa Mwidhiniwa | 15. | 1) Afisa mwidhiniwa anaweza kutoa amri ya kuzuia shughuli yoyote isifanyike kama vile utengenezaji wa vyakula, pombe, mijumuiko, sherehe na mikusanyiko yoyote kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi, au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuli hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu.<br><br>2) Vyakula, vyombo na vifaa vingine vyovyote vitakavyokamatwa baada ya kutolewa amri ya kuzuia kufanyika kwa shughuli hiyo ambavyo vitakuwa vimetumika kutunzia, kubebea, kuhifadhia na kusafirishia vitaharibiwa kwa gharama za mmiliki na Halmashauri haitahusika na gharama zozote zitakazotokea wakati wa utekelezaji wa zoezi ama amri hiyo.<br><br>3) Afisa mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kumwandikia mtu yeyote barua ya wito wa kumtaka kufika ofisini kwa ajili ya kutoa maelekezo kuhusiana na usafi. |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| | | 4) Afisa mwidhiniwa anaweza kuzuia kibali cha kuendesha biashara ya hoteli, hosteli na biashara nyinginezo mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti ya kiafya yaliyotolewa na Halmashauri.<br><br>5) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote wakati wowote kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>6) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuagiza kufungwa kwa biashara yoyote au jengo ambalo halijakaguliwa au lililokaguliwa na kukutwa limekiuka kanuni na masharti ya afya.<br><br>7) Afisa mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa adhabu ya papo kwa papo kwa mtu yeyote atakayekutwa amechafua mazingira na amekwenda kinyume na Sheria Ndogo hizi. |
| Machinjio na maduka ya nyama | 16. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama (Butcher) kuhakikisha kwamba:<br><br>a) Ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi 6 kutoka usawa wa sakafu.<br>b) Lina maji safi, magogo na misumeno ya kukatia nyama na vyuma vya kutundikia nyama.<br>c) Lina kabati ya vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na mizani ya kupimia nyama.<br>d) Kuna pipa au kifaa cha kuhifadhia takataka.<br>e) Muuzaji avae Apron nyeupe, kofia nyeupe na gumboot.<br>f) Muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita.<br>g) Kuna karo la maji machafu.<br><br>2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja, au kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa machinjio au maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri.<br><br>3) Ni marufuku kuuza nyama isiyo kaguliwa na mtaalam wa mifugo au mtaalam wa Afya.<br><br>4) Ni marufuku kusafirisha nyama toka machinjioni bila kutumia gari maalum la kusafirishia nyama lililoidhinishwa na Halmashauri. |
| Ufugaji | 17. | 1) Ufugaji unaoruhusiwa ni ule ambao hauleti kero kwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | majirani na athari za kimazingira yaani ufugaji wa ndani (*zero grazing*) kwenye zizi na kwa kuzingatia idadi ya mifugo inayoruhusiwa au katika maeneo yaliyotengwa kama malisho ya mifugo.<br><br>2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuacha mifugo au kusababisha mifugo kuachwa kuzurura ovyo mitaani, barabarani au kuchungwa kwenye eneo lolote lisiloruhusiwa.<br><br>3) Halmashauri itatoza faini kwa mifugo yote inayozurura maeneo ya mjini kama ilivyoainsishwa kwenye jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.<br><br>4) Ni wajibu wa kila mfugaji kuhakikisha kwamba sehemu anayotumia inakuwa katika hali ya usafi wakati wote kwa kukusanya uchafu wowote utokanao na wanyama kama vile kinyesi, manyoya na nyasi au mabaki ya vyakula na kwenda kutupwa kwenye dampo au kupelekwa shambani kama mbolea. |
| Uendeshaji wa biashara ya hoteli, hostel na migahawa | 18. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni na hosteli au nyumba za biashara kuhakisha anapata kibali kutoka Halmashauri kabla hajaanza biashara na kukaguliwa na Afisa afya kuona kama masharti na kanuni za Afya zimezingatiwa.<br><br>2) Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, mgahawa, Hoteli na Hosteli kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa mahitaji yafuatayo yamezingatiwa:-<br>a) mwanga na hewa ya kutosha;<br>b) nafasi na vifaa (samani) za kutosha;<br>c) uimara wa jengo;<br>d) mfumo wa uondoshaji wa maji taka, miminika na taka ngumu;<br>e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;<br>f) utoshelezaji wa vyoo na mabafu kwa jinsia zote;<br>g) vifaa vya zima moto;<br>h) tanki la kuhifadhia maji safi;<br>i) vyoo na bafu vimesakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita toka usawa wa sakafu;<br>j) Uwepo wa vyandarua ili kuzuia mbu kwenye hosteli na nyumba za kulala wageni; na<br>k) Nyumba za kulala wageni zinapaswa kutumia shuka safi nyeupe katika kutandika kitanda. |
| Upimaji wa | 19. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki kuhakikisha mhudumu wa |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| afya | | hoteli, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayeuza au anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza wamepima afya zao kila baada ya miezi sita.<br><br>2) Mmiliki yeyote atakayeruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi laki mbili (200,000/=) na mhudumu mwenyewe pia atalipa faini isiyozidi elfu hamsini (50,000/=). |
| Ada ya ukaguzi wa afya | 20. | 1) Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya ambayo italipwa kwa mwaka kabla ya mwombaji kupewa leseni ya biashara.<br><br>2) Viwango vya ada ya ukaguzi wa afya vitakuwa kama vilivyoainishwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.<br><br>3) Ada ya ukaguzi wa afya italipwa kila mwaka wakati wa kuhuisha leseni ya biashara. |
| Wajibu wa Halmashauri | 21. | 1) Halmashauri itatenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka (dampo) na kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji hadi kwenye dampo, viwango vya malipo ni kama vilivyoainishwa kwenye jedwali la tatu la sheria ndogo hizi.<br><br>2) Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii (CBOs) na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mikataba na Halmashauri.<br><br>3) Halmashauri itaelekeza halmashauri za vijiji vyote kutenga maeneo kwa ajili ya kuhifadhia maji taka |
| Maji taka | 22. | 1) Kila mmiliki wa nyumba anatakiwa kuhakikisha kuwa ana karo la kuhifadhi maji taka na atawajibika kunyonya maji taka pale karo linapojaa.<br><br>2) Ni marufuku kutitirisha au kuelekeza maji, kutoka vyooni, bafuni, karoni, baada ya kufua au kuosha vyombo kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhi maji taka. |
| Taka za viwanda | 23. | 1) Ni marufuku kwa kiwanda chochote kutoa au kusababisha kutoa uchafu wa aina yoyote, maji machafu au harufu mbaya na kusababisha kero kwa wakazi wa |

RASMU

| | | |
|---|---|---|
| | | eneo la Halmashauri.<br><br>2) Ni wajibu wa kila mwenye kiwanda kuhakikisha kuwa taka kama vile vumbi, maganda, moshi na takataka nyingine zinazoweza kuleta kero au adha kwa ujumla haziwafikii wala hazileti madhara kwa binadamu na viumbe wengine hai. |
| Uendeshaji wa viwanda | 24. | 1) Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kubangua korosho, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi. |
| Uteuzi wa wakala | 25. | 2) Halmashauri inaweza kuteua kampuni, kikundi, kikundi cha jamii kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hizi. |
| Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia | 26. | 1) Ni wajibu wa kila mmiliki wa nyumba au jengo lolote la biashara kuhakikisha kwamba nyumba yake ina choo safi, imara na madhubuti kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo na kuhakikisha kinatumika wakati wote.<br><br>2) Choo kitahesabiwa kuwa kimejaa kama kitabaki futi tatu kutoka kwenye kinyesi kufika kwenye tundu au mlango wa shimo.<br><br>3) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini (60) kutoka kisima au chanzo chochote cha maji kinachotumika kwa matumizi ya nyumbani. |
| Vyoo vya umma | 27. | 1) Halmashauri inaweza kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au Taasisi kujenga vyoo vya Umma (Public toilet) katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.<br><br>2) Vyoo hivyo vitamilikiwa na Halmashauri au kwa ubia na wajenzi na vitakuwa ni vya kulipia kama itakavyokuwa imeelekezwa na Halmashauri katika mkataba wake na mawalaka watakaopewa kusimamia vyoo hivyo.<br><br>3) Ni wajibu wa mtu, kikundi, Taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa madhumuni ya ujenzi, sherehe au sehemu yoyote ambayo itakutanisha watu kwa muda maalum endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.<br><br>4) Kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo kadri atakavyoelekezwa na Afisa mwidhiniwa |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| | | vyenye viwango vinavyokubalika chini ya Sheria Ndogo hizi kwa ajili ya matumizi ya jinsia za kike na kiume, ikiwa ni pamoja na mifereji ya haja ndogo kwa wanaume (urinal). |
| Ilani ya kujenga choo | 28. | 1) Endapo katika ukaguzi wa Afya itagundulika kuwa nyumba yoyote ya makazi au jengo lolote la biashara halina choo, choo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, ilani ya siku 14 ya kurekebisha choo hicho itatolewa.<br><br>2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa. |
| Ilani ya kuondoa kero | 29. | 1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba (7) kwa mmiliki wa nyumba au jengo la biashara mpangaji, mtumiaji, na au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo. |
| Ada ya uzoaji taka | 30. | 1) Halmashauri itakusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kutupa taka za majumbani na biashara kwa kulipia kama ilivyoainishwa kwenye jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi. |
| Makosa | 31. | 1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:<br><br>a) Atamzuia au kujaribu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;<br>b) Atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hizi;<br>c) Atamwaga takataka katika mtaa, mtaro wa maji ya mvua, uchochoroni, nyumbani, eneo la biashara au mahali popote hadharani au katika eneo lolote la wazi bila idhini ya Halmashauri;<br>d) Atatupa hovyo maganda ya matunda ya aina yote, pipi, biskuti, vipisi vya sigara, chocolate, miwa na aina nyingine ya maganda;<br>e) Kwa makusudi ataacha kutoa taarifa za mtu au taasisi yoyote itakayomwaga takataka kwenye maeneo yasiyoruhusiwa;<br>f) Ataendesha biashara ya pombe ndani ya nyumba ya makazi;<br>g) Atatirirsha maji machafu barabarani au katika eneo la nyumba ya jirani;<br>h) Ataosha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| | | dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa, lambo au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;<br>i) Atauza vyakula vilivyopikwa barabarani au nje ya majengo mengine bila kibali;<br>j) Atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, kuendesha shughuli za viwanda katika maeneo ya wazi, makazi, barabarani, uchochoroni, au katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo bila kuzingatia taratibu za mipango miji;<br>k) Ataanzisha au kufungua karakana katika majengo au majumba au maeneo ya makazi;<br>l) Ataenda haja ndogo au kubwa kwenye sehemu isiyo rasmi;<br>m) Atashindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;<br>n) Atafungua jengo la biashara bila kukidhi matakwa ya Afya;<br>o) Atauza bidhaa au vyakula vilivyokwisha muda wake;<br>p) Mifugo yake itazurura au kuswaga ovyo maeneo ya mjini;<br>q) Hatashiriki kufanya usafi siku zilizopangwa;<br>r) Atasafirisha nyama toka machinjioni bila kutumia gari maalum la kusafirishia nyama;<br>s) Atashindwa kujenga na kutumia choo bora; na<br>t) Atashindwa kutekeleza ilani ya kuondoa kero. |
| Kufifilisha kosa | 32. | 1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifisha kosa kwa kumtoza faini mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi kiasi kisichopungua shilingi Laki Mbili (200,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye jedwali la nne la sheria ndogo hizi na atatakiwa kulipa tozo anayodaiwa au kutekeleza wajibu wake. |
| Adhabu | 33. | 1) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi Laki Mbili (200,000/=) na isiyozidi Milioni Moja (1,000,000/=) au kifungo kisichozidi mwaka mmoja au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo. |

RASMU

## JEDWALI LA KWANZA

*Limetengenezwa Chini ya Kifungu cha 17(3)*

## VIWANGO VYA FAINI KWA MFUGO AU MIFUGO INAYOZURURA OVYO NDANI YA ENEO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

| Na. | Aina ya Mifugo | Adhabu/faini(Tshs) kwa kila mfugo |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 50,000/= |
| 2. | Mbuzi | 20,000/= |
| 3. | Kondoo | 20,000/= |
| 4. | Nguruwe | 20,000/= |
| 5. | Mbwa | 50,000/= |
| 6. | Punda | 20,000/= |
| 7. | Ngamia | 20,000/= |

## JEDWALI LA PILI
## ADA YA UKAGUZI WA AFYA

*Limetengenezwa chini ya Kifungu cha* **20(2)**

| NA | AINA YA BIASHARA | ADA KWA MWAKA |
|---|---|---|
| 1. | Baa na maduka ya vinywaji (groceries) | 20,000 |
| 2. | Migahawa, baba na mama lishe | 10,000 |
| 3. | Nyumba za kulala wageni (guest house na hosteli) | 20,000 |
| 4. | Kumbi za starehe na mikutano | 20,000 |
| 5. | Maduka ya jumla na rejereja | 15,000 |
| 6. | Gereji | 15,000 |
| 7. | Majengo mengine ya biashara | 10,000 |
| 8. | Kupima afya za wauza vyakula | 10,000 |

RASIMU

**JEDWALI LA TATU**

***Limetengenzwa Chini ya kifungu cha 30***

## ADA YA UZOAJI TAKA

| NA | ENEO | KIWANGO KWA MWEZI |
|---|---|---|
| 1. | Makazi (kwa kaya) | 2,000/= |
| 2 | Nyumba za kulala wageni | 5,000/= |
| 3 | Migahawa, baba, mama lishe | 3,000/= |
| 4 | Kituo cha Afya | 10,000/= |
| 5 | Zahanati (Taka zisizo hatarishi) | 5,000/= |
| 6 | Hospitali (Taka zisizo hatarishi) | 15,000/= |
| 7 | Duka la dawa | 2,000/= |
| 8 | Kiwanda kidogo | 10,000/= |
| 9 | Kiwanda kikubwa | 100,000/= |
| 10 | Karakana/gereji za pikipiki | 3,000/= |
| 11 | Gereji za magari<br>a) Ndogo<br>b) Kubwa | <br>5,000/=<br>10,000/= |
| 12 | Fundi seremala | 3,000/= |
| 13 | Fundi chuma | 3,000/= |
| 14 | Duka la jumla | 5,000/= |
| 15 | Duka la rejareja | 3,000/= |
| 16 | Grocery | 4,000/= |
| 17 | Bar | 3,000/= |
| 18 | Pombe za kienyeji | 3,000/= |
| 19 | Kumbi za sherehe | 5,000/= |
| 20 | Duka la kuuza nyama/samaki | 4,000/= |
| 21 | Genge au duka dogo la chakula | 3,000/= |
| 22 | Dobi | 3,000/= |
| 23 | Saloon | 6,000/= |
| 24 | Kituo cha kuuza mafuta | 10,000/= |
| 25 | Fundi nguo | 2,000/= |
| 26 | Ghala | 5,000/= |
| 27 | Mashine za kukoboa, kusaga na kusindika nafaka<br>a) Ndogo<br>b) Kubwa | <br>3,000/=<br>5,000/= |
| 28 | Nyumba za video/sinema | 3,000/= |
| 29 | Karakana ya utengenezaji wa samani | 5,000/= |
| 30 | Ofisi ya taasisi za kidini | 3,000/= |
| 31 | Ofisi ya Taasisi zisizo za kidini | 5,000/= |
| 32 | Uwanja wa michezo | 5,000/= |
| 33 | Mashine za kusaga na kukoboa:<br>a) Ndogo | <br>3,000/= |

RASIMU

| | | |
|---|---|---|
| | b) Kubwa | 5,000/= |
| 34 | Sehemu za kuoshea magari/pikipiki | 5,000/= |
| 35 | Stationary | 2,000/= |
| 36 | Taasisi Ndogo za Fedha na mawakala | 2,000/= |
| 37 | Taasisi kubwa za Fedha (kama vile CRDB, NMB, TACOBA, PBZ na zingine zinazofanana nazo) | 10,000/= |

**JEDWALI LA NNE**

***Limetengenezwa Chini ya Kifungu cha 31***

**VIWANGO VYA FAINI KWA MAKOSA MBALIMBALI YANAYOTOKANA NA UKIUKWAJI WA SHERIA ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA**

| Na. | Aina ya kosa | Adhabu/faini(Tshs) kwa kila mfugo |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba au jengo la biashara, nyumba ya ibada, majengo ya taasisi kutokuwa na choo au choo kilichobomoka au kukosa sifa ya kuwa choo bora | 50,000/= |
| 2. | Nyumba kukosa kichanja | 10,000/= |
| 3. | Kutiririsha maji machafu ovyo au kwenye mifereji ya maji ya mvua/kutosafisha mifereji | 50,000/= |
| 4. | Nyumba kuwa chafu au kuzungukwa na majani au utupaji ovyo wa takataka | 50,000/= |
| 5. | Kutopima afya watoa huduma wa vyakula na vinywaji | 50,000/= |
| 6. | Kutokuwa na shimo la taka | 20,000/= |
| 7. | Kunya au kukojoa mahali ambapo siyo choo | 50,000/= |
| 8. | Kutupa taka eneo kando ya barabara | 100,000/= |

RASMI

**KUFIFILISHA KOSA**
***(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 32)***

Mimi……………………………………….nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………..Mwaka nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha……………….cha sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa za mwaka 2025.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kutekeleza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi pamoja na kulipa faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO YA HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe……………………………….. Mwezi…………………Mwaka…………………

Jina……………………………………….Saini……………………………………….

Mbele ya:
Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini……………………………………….Tarehe……………………………………